FUNZO LA 5

1. Malaika wote walitoka wapi?
-Mungu aliwaumba wote hapo mwanzo.

2. Mungu alipowaumba malaika, je, Mungu aliwapa mwili na damu?
-La.
-Mungu aliumba malaika kama roho.

3. Kwa nini Mungu aliumba malaika?
-Mungu aliumba malaika ili wampende.
-Mungu aliumba malaika ili wamtii.
-Mungu aliumba malaika ili wamtumikie.

4. Je, Mungu aliumba malaika wazuri au wabaya?
-Mungu aliumba malaika wote, wazuri.

5. Mungu aliumba malaika wangapi?
-Mungu aliumba malaika wengi, hatuwezi kuwahesabu wote.

6. Hapo mwanzo, malaika wote waliishi wapi?
-Mbinguni pamoja na Mungu.

7. Jina la malaika aliyeumbwa na hekima kubwa na urembo mwingi ni?
-Lusifa.

8. Je, Mungu alimuumba Lusifa mzuri au mbaya?
-Mzuri.



-Mungu anaweza kuumba malaika wazuri tu.

9. Hapo mwanzo, nini kilimfanyikia Lusifa?
-Lusifa aliona hekima na urembo wake, akajawa na kiburi na akataka kumtoa Mungu mamlakani.

10. Ni nani aliyekuwa wa kwanza kutenda dhambi?
-Lusifa.

11. Je, Mungu alijua kuwa Lusifa alitaka kumtoa mamlakani?
-Ndiyo.
-Mungu aliyajua mawazo yote maovu ya Lusifa.

12. Je, Mungu alimruhusu Lusifa kumtoa mamlakani?
-La.

13. Kwa sababu Lusifa alikuwa wa kwanza kutenda dhambi, Mungu alibadilisha jina la Lusifa. Jina mpya la Lusifa ni nani?
-Shetani.

14. Jina la Shetani linamaanisha nini?
-Jina la Shetani linamaanisha “adui.”

15. Mungu alimwadhibu vipi Shetani kwa kutenda dhambi?
-Mungu alikasirishwa na Shetani, akamwondoa mbinguni.

16. Kwa sababu malaika walio mfuata Shetani walimkosea Mungu, Mungu alibadilisha majina yao. Je hao malaika waliomfuata Shetani waliitwaje?
-Mapepo.

17. Mungu aliwaadhibu aje mapepo waliomfuata Shetani?
-Mungu alikasirishwa nao, akawaondoa mbinguni.

18. Tena Mungu aliwaadhibu vipi Shetani na mapepo wake?
-Mungu aliandaa mahali pabaya pa adhabu ya milele kwa Shetani na mapepo wake.

19. Jina la mahali pa adhabu ya milele ni?
-Ziwa la moto wa milele.

20. Shetani na mapepo wake wanaishi wapi sasa?
-Shetani na malaika wake wanaishi duniani sasa.

21. Shetani na mapepo wake wanafanya nini sasa?
-Wanapingana dhidi ya kazi ya Mungu mchana na usiku.

-Wacha tusome tena maneno ya kwanza ya Mungu katka kitabu chake:

Tusome Mwanzo 1:1

1-Hapo mwanzo, Mungu aliziumba mbingu na nchi.

-Mwanzo ni lini?

-Mwanzo ni kitambo sana, wakati Mungu alipoumba vitu vyote.

-Hapo mwanzo, nani aliyeumba vitu vyote vilivyomo ulimwenguni?



-Mungu.

-Kila kitu kilicho ulimwenguni kiliumbwa na Mungu hapo mwanzo.

-Ni nini kilichokuwa ulimwenguni kabla ya Mungu kuumba vitu vyote?
-Hakuna.

-Kama hakukuwa na chochote, basi Mungu alitumia nini kuumba vitu vyote?

-Mungu alitumia nini kuumba dunia na anga?

-Mungu alitumia nini kuumba jua, mwezi na nyota?

-Kama hakungekuwa miti, wanaume mngeweza kujenga nyumba?
-La.

-Je, wanaume mngeweza kujenga nyumba bila chochote?
-La.

-Kama hakungekuwa matope, je, wanawake wangeweza kufinyanga vyungu?
-La.

-Wanawake mgeweza kufinyanga vyungu bila matope?
-La.

-Kama hakukuwa udongo, je, nyinyi watoto mngetengeneza mwanasesere?
-La.

-Je, watoto mngeweza kutengeneza mwanasesere bila chochote?
-La.

-Kama hakukuwa na chochote, basi Mungu alitumia nini kuumba vitu vyote?
-Hakuna.

-Kwa hivyo Mungu aliumba vipi ulimwengu?

-Mungu aliumba ulimwengu bila chochote.

-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho mtakatifu waliumba kila kitu bila chochote.

-Mungu aliwezaje kuumba mbingu na nchi bila chochote?

-Mungu aliwezaje kuumba kila kitu kutoka kwa kisichokuwepo?

-Mungu ni mwenye nguvu zote.

-Nguvu za Mungu haziishi.
-Nguvu za Mungu ni za milele.

-Je, kuna kipimo cha nguvu za Mungu?



-La.

-Hakuna kipimo dhidi ya nguvu za Mungu.
-Hakuna mwisho kwa nguvu za Mungu.

-Hakuna asichoweza kufanya Mungu.
-Mungu anaweza kufanya chochote.

-Mungu aliumba ulimwengu wote bila chochote.

-Je, kuna aliye na nguvu zaidi ya Mungu?
-La.

-Je, Shetani ana nguvu zaidi ya Mungu?
-La.

-Je, mapepo wa Shetani wana nguvu zaidi ya Mungu?
-La.

-Je, watu wana nguvu zaidi ya Mungu?
-La.

-Kuna chochote ambacho Mungu hawezi fanya?
-La.

-Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka.
-Mungu anaweza kufanya kila kitu anachotaka kufanya.

-Je, Mungu alijuaje jinsi ya kuumba kila kitu bila chochote?

-Je, Mungu alifundishwa na mtu kuumba kila kitu?

-Wanaume mnawafundisha wana wenu jinsi ya kupanda mahindi, kwa sababu hawajui jinsi ya kupanda mahindi.

-Wanawake mnawafundisha wasichana jinsi ya kupika, kwa sababu hawajui kupika.

-Je, Mungu alifundishwa na mtu kuumba kila kitu?
-La.

-Kwa nini hakuna aliyemfundisha Mungu?

-Kwa sababu hapo mwanzo, hakukuwa na yeyote ambaye angemfundisha Mungu.

-Kama Mungu pekee ndiye aliyekuwepo kabla ya mwanzo, hakukuwa na mwingine wa kumfundisha.

-Pia Mungu haitaji kufundishwa.

-Kwa nini Mungu haitaji kufundishwa na yeyote?

-Kwa sababu Mungu anajua yote.

-Hekima ya Mungu haiishi.
-Hekima ya Mungu ni ya milele.

-Je, kuna kipimo kwa hekima ya Mungu?
-La.



-Hakuna kipimo dhidi ya hekima ya Mungu.
-Hekima ya Mungu haina mwisho.

-Hakuna lolote asilolijua Mungu.
-Mungu anajua kila kitu.

-Mungu aliumba ulimwengu wote bila chochote.

-Je, kuna aliye na hekima zaidi ya Mungu?
-La.

-Je, Shetani ana hekima zaidi ya Mungu?
-La.

-Je, mapepo ya Shetani yana hekima zaidi ya Mungu?
-La.

-Je, watu wana hekima zaidi ya Mungu?
-La.

-Mungu anajua kila kitu kuhusu kila kitu.

-Hii ndiyo sababu ya kuyasikiliza maneno ya Mungu.